# KATC Taarifa

*Umwagiliaji Maji Mashambani Kwa Maendeleo ya Kilimo*

Toleo na. 3 Julai-Septemba 2004



**WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA**
**KILIMANJARO AGRICULTURAL TRAINING CENTRE (KATC)-MOSHI**
**S.L.P 1241 MOSHI– Simu 255-27-2752293**
**barua pepe: katc@kilionline.com**


## KATC yafanya tathmini ya mafunzo ya msimu wa kwanza katika skimu za mfano

*R.J. Shayo**

Mradi wa KATC awamu ya pili unatekelezwa katika skimu sita hapa nchini na skimu nne katika nchi jirani za Kenya, Malawi,Uganda na Zambia, lengo likiwa ni kuinua kiwango cha uzalishaji wa zao la mpunga kwa njia ya umwagiliaji ili kuzifanya skimu hizo kuwa za mfano kwa skimu nyingine.

Mbinu inayotumika kufikia lengo hilo ni mafunzo kwa wakulima na watendaji katika skimu hizo yakizingatia ufumbuzi wa matatizo ya wakulima yaliyoibuliwa kwa kutumia mbinu shirikishi jamii.

Kwa kipindi cha miezi isiyopungua mitano Mradi wa KATC awamu ya pili umekuwa ukifanya tathmini ya mafunzo ya msimu wa kwanza yaliyoendeshwa chuoni KATC na katika skimu 5 za umwagiliji kwa wakulima viongozi na wa kati.

Katika tathmini hiyo ilibainika kuwa hatua kubwa ya uzalishaji imeweza kufikiwa katika viwango tofauti kwa kila skimu. Wakulima viongozi na wakulima wa kati ndio waliopata viwango vya kuvutia katika uzalishaji wa zao la mpunga.

Baadhi ya matokeo ya msimu wa kwanza -2004 ukilinganisha na msimu wa 2003 kwa skimu za Mombo na Nakahuga ni kama ifuatavyo:

| Viashiria | Mombo | | Nakahuga | |
|---|---|---|---|---|
| | 2003 | 2004 | 2003 | 2004 |
| Mavuno (kilo/he) | 3,799 | 4,532 | 3,095 | 4,443 |
| Pato kwa familia(sh) | 273,463 | 318,854 | 100,337 | 211,575 |

Aidha wakulima viongozi na wa kati kwa viwango tofauti waliweza kutumia mbinu mbalimbali walizojifunza katika mashamba yao na hivyo kuweza kuboresha kilimo chao kwa kiwango cha kuridhisha. Wapo pia baadhi ya wakulima wengine ndani ya skimu ambao wameweza kujifunza kutoka kwa wakulima wenzao na kuweza kutumia baadhi ya mbinu bora za kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji kwenye mashamba yao.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali Mhe. Msagama Ndololo akiwatunukia vyeti vya pongezi Wakulima Viongozi wa Skimu ya Mbuyuni katika sherehe ya wakulima iliyofanyika katika kijiji cha Mabadaga

Kwa ujumla tekinolojia hii ya kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji imeendelea kuenea na kupokelewa katika viwango tofauti kati ya skimu moja na nyingine.

Hata hivyo, licha ya mafanikio hayo ya kutia moyo, pia yapo matatizo kadhaa yaliyoibuliwa wakati wa tathmini ambayo yamechangia katika kushindwa kufikia malengo ya uzalishaji. Matatizo yaliyo mengi yanafanana jingawaje zipo tofauti katika viwango vya ukubwa na uzito wa tatizo lenyewe. Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na:

- Baadhi ya wakulima kutofuata kalenda ya msimu
- Upungufu wa maji ya umwagiliaji kutokana na matumizi mabaya ya maji na ubovu wa miundo mbinu.
- Mahudhurio yasiyoridhisha ya baadhi ya wakulima viongozi na wakulima wa kati katika mafunzo
- Udhaifu katika uenezaji wa tekinolojia kutoka kwa wakulima viongozi kwenda kwa wakulima wa kati na kutoka kwa wakulima wa kati kwenda kwa wengine.
- Udhaifu wa vyama vya wamwagiliaji katika kusimamia majukumu mbalimbali

Baada ya kubaini matatizo hayo wakulima walipata fursa ya kuandaa mkakati wa utekelezaji kwa msimu wa pili ambao ndio utakaokuwa dira ya kufikia malengo ya kila skimu.

Pamoja na mambo mengine, pongezi nyingi zilitolewa kwa wadau wote wa mradi wa KATC awamu ya pili wakiwemo Wakulima wa kati, wakulima wengine, KATC na Halmashauri za wilaya kwa juhudi walizozionyesha. Pongezi hizo zilifuatiwa na kuwatunukia vyeti vya pongezi wakulima viongozi na wataalamu wa skimu walioonyesha bidii katika utekelezaji wa majukumu yao.

*Mkuu wa Chuo-KATC

__Yaliyomo katika toleo hili:__


Wilaya ya Songea yachangia skimu ya Uk. 2
Mkuu wa Wilaya kushirikiana na Uk. 2
Mwega watakiwa kuongeza bidii katika uzalishaji Uk. 3
Hawavumi lakini wamo !!! Uk. 3
Jinsi ya kuandaa mbegu za mpunga Uk. 4

# Wilaya ya Songea Vijijini yachangia milioni 54 katika kuboresha skimu ya umwagiliajia ya Nakahuga.

Mojawapo ya wadau muhimu wa mradi wa KATC awamu ya pili ni Halmashauri za wilaya ambazo skimu sita zinazoandaliwa kuwa za mfano zipo. Licha ya kuwa wadau muhimu vilevile ndio wahimili wakuu wa skimu hizo za umwagiliaji.

Halmashauri hizo za wilaya ni pamoja na Halmashauri ya wilaya ya Korogwe, Igunga, Kilosa, Mbarali, Songea na Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga ambazo zimeshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuziendeleza kwa hali na mali skimu za umwagiliaji zilizochaguliwa ili kufanikisha lengo la kuzifanya kuwa za mfano na kuweza kutumiwa kama kituo cha mafunzo kwa ajili ya skimu nyingine katika wilaya husika na kanda nzima ya umwagiliaji katika uboreshaji wa kilimo cha mpunga na mazao mengine kwa njia ya umwagiliaji.

Katika kutekeleza majukumu yake kama mdau Halmashauri ya wilaya ya Songea imeweza kutoa mchango mkubwa katika kuchangia gharama za mafunzo pamoja na kuiendeleza skimu ya Nakahuga. Katika mkutano wa wadau wote wa mradi wa KATC awamu ya pili, Mkurugenzi mtendaji wa wilaya hiyo katika taarifa yake iliyowasilishwa kwa niaba yake na meneja wa skimu ya Nakahuga



Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya ya Songea Vijijini akielezea jambo katika warsha ya wadau wa Mradi wa KATC II

Ndugu Malya; alieleza kuwa jumla ya shilingi millioni 54 zimetolewa na kutumika katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya skimu ya Nakahuga katika msimu wa kwanza wa mafunzo. Pamoja na mambo mengine muhimu fedha hizo zimetumika katika;

- kuchangia gharama za vyakula na vinywaji wakati wa siku/sikukuu za wakulima,
- kuwawezesha wataalamu wa wilaya wakati wa mafunzo na shughuli za ufuatiliaji katika skimu,

kuwasafirisha wakulima wa kutoka skimu nyingine za umwagiliaji kwenda Nakahuga kwa ajili ya mafunzo.

Vilevile wilaya imeweza kuisaidia skimu katika;

- ujenzi wa banio na mfereji mkuu,
- upatikanaji na usafirishaji wa pembejeo za kilimo pamoja na

kuboresha mawasiliano ya barabara kati ya Kijiji cha Morogoro-Peramiho na Nakahuga.

Aidha taarifa hiyo ilieleza kuwa wilaya itaendelea kuisadia skimu ya Nakahuga kwa kushirikiana kwa karibu na mradi wa KATC awamu ya pili ili kufikia lengo lililowekwa.

Hatua hiyo ya Halmashauri ya wilaya ya Songea imekuwa kichocheo kikubwa cha ufanisi kwa wakulima wa skimu ya Nakahuga ambao wamekuwa mstari wa mbele kuchangia nguvu zao katika kuiboresha skimu yao na kuzalisha zaidi.



Wakulima wakiangalia mashamba ya mpunga ya wulima viongozi katika skimu ya Nakahuga

# Mkuu wa wilaya kushirikiana na Skimu ya Mbuyuni.

Mkuu wa wilaya ya Mbarali Mheshimiwa Msagama Ndololo ameahidi kushirikiana bega kwa bega na wakulima wa skimu ya umwagiliaji ya Mbuyuni ili kuhakikisha kuwa skimu hiyo inakuwa ya mfano katika kanda ya umwagiliaji ya Mbeya kama ilivyokusudiwa na mradi wa taifa wa KATC awamu ya pili. Ahadi hiyo ilitolewa wakati wa maadhimisho ya sikukuu ya wakulima iliyofanyika katika kijiji cha Mabadaga katika skimu ya Mbuyuni tarehe 9/7/2004.

Katika kuhakikisha malengo ya uzalishaji ya skimu hiyo ambayo ni kuzalisha wastani wa tani 6 za mpunga kwa hektari, Mkuu wa wilaya alisema kuwa yupo tayari kushirikiana na idara ya kilimo wilaya pamoja na uongozi wa ushirika wa umwagiliaji maji wa skimu ya Mbuyuni katika kutekeleza mkakati wa utekelezaji wa msimu wa pili waliojiwekea. Baadhi ya masuala yanayohitaji kutiliwa mkazo zaidi ni pamoja na:



Wakulima viongozi na wa kati wa Skimu ya Mbuyuni wakiigiza wakati wa sherehe za wakulima

- kuboresha mahudhurio ya wakulima viongozi na wa kati katika mafunzo
- kuwa na wakulima viongozi na wa kati wanaojituma katika kutekeleza mbinu za uzalishaji walizofundishwa na
- kuhakikisha kuwa tekinolojia ya kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji inaenezwa kwa wakulima wengine ndani na nje ya skimu (katika kanda ya Mbeya)

Katika sikukuu hiyo Mkuu wa wilaya aliwatukia vyeti vya pongezi wakulima viongozi waliofanya vizuri katika msimu wa kwanza.



Mkulima kiongozi akielezea mafanikio aliyoyapata wakati wa sikukuu ya wakulima

## Mkuu wa mkoa awataka wakulima waongeze bidii.

Mkuu wa mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Steven Mashishanga katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Afisa mipango kutoka sekretarieti ya mkoa Ndugu Kikwesha aliwahimiza wakulima wa skimu ya Mwega kuongeza bidii zaidi katika uzalishaji wa mazao kwa njia ya umwagiliaji. Wakulima wa skimu ya Mwega wamebahatika kuwa na mradi mkubwa wa umwagiliaji wenye miundo mbinu ya kisasa hivyo hawana budi kubadilika katika uzalishaji kwa kuzingatia na kutekeleza mafunzo ya kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji wanayoyapata. Ilieleza hotuba hiyo.

Katika kusherehekea sikukuu ya wakulima baada ya kumaliza msimu wa kwanza wa mafunzo yalioendeshwa na mradi wa taifa wa KATC awamu ya pili, Mkuu wa mkoa alisema kuwa kwa kuongeza uzalishaji anategemea kuona wakulima wa bonde la Mwega wanaboresha maisha yao kwa kujijengea nyumba bora za kuishi na kujenga shule za sekondari kwa ajili ya watoto wao na vizazi vijavyo.



Bw. Kikwesha (Afisa mipango wa Mkoa wa Morogoro) akiwahutubia wakulima wa Mwega wakati wa sherehe za wakulima

## Skimu ya Mwamapuli wachangia chakula katika mafunzo.

Katika kutekeleza sera ya uchangiaji gharama katika mafunzo yanayotolewa na mradi wa KATC awamu ya pili, wakulima wa Skimu ya umwagiliaji ya Mwamapuli wameweza kuonyesha mfano wa kuigwa baada ya kuweza kuchangia chakula kilichotumika kwa wakulima katika mafunzo yote ya siku 5 ya awamu ya 3 pamoja na siku 4 za tathimini iliyofanyika katika skimu hiyo.

Skimu ya Mwamapuli imekuwa ya pili kwa uchangiaji baada ya Skimu ya Nakahuga ambayo imekuwa ikichangia chakula katika mafunzo yote yaliyofanyika ndani ya skimu yao.

Zoezi hilo lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa baada ya Chama cha ushirika cha wakulima wa Mwamapuli chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mzee



Kinamama wa Skimu ya Mwamapuli wakishiriki katika mapishi wakati wa mafunzo

Ngula kuwahamasisha wakulima na kusimamia kwa makini suala hilo.

Pamoja na uchangiaji wa chakula, ushirika huo uliweza kugharamia shughuli zote za upishi ikiwa ni pamoja na kuwalipa wapishi, ununuzi wa kuni na usombaji wa maji.

KATC iliweza kuchangia kwa kuongezea sehemu ambazo zilionyesha upungufu pamoja na gharama nyingine za mafunzo kwa ujumla.

Hakika mfano huu wa uchangiaji unafaa kuigwa na skimu nyingine za umwagiliaji katika kutekeleza sera hii ya kujivunia ya uchangiaji gharama na kuondokana na dhana potofu ya utegemezi.

## Hawavumi lakini wamo.........hongera wakulima wa kati !!!

Nii kweli kabisa kuwa katika utekelezaji wa mafunzo yanayotolewa Mradi wa KATC awamu ya pili wapo wakulima wengi walioonyesha juhudi kubwa na kufanikiwa kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga ukilinganisha na ilivyokuwa awali.

Ingawa wakulima viongozi ndio walioonekana kuonyesha juhudi katika kutekeleza kwa vitendo mafunzo waliyoyapata kama kina Bi. Hadija Ismaili, Shufaa Mhando, Rainery Mapunda, Pius Myonga, Magdalena Kilyunguma, Abbas Mkwama na wengineo lakini wapo wakulima wa kati na hata wakulima wengine waliofanya vizuri katika msimu wa kwanza.



Mmoja wa wakulima wa kati wa Skimu ya Mombo akishona magunia ya mpunga baada ya kupata mavuno mazuri katika shamba lake

Baadhi ya wakulima hao wa kati ni pamoja na Ndugu Thadei Mwikonzi wa Skimu ya umwagiliaji ya Mwega ambaye alionyesha juhudi kubwa katika kuonyesha kwa vitendo mbinu mbalimbali za kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji alizojifunza katika shamba lake. Mbinu alizotumia ni pamoja na utengenezaji wa kingo imara za majaruba ya mpunga, kusawazisha shamba lake kwa kutumia zana rahisi pamoja na mbinu nyingine nyingi.



Bw. Thadei Mwikonzi wa Skimu ya Mwega akimwonyesha Bwanashamba wake mafanikio ya shamba lake.

Juhudi za mkulima huyo zilimwezesha kuwa na mazao yaliyostawi vizuri na hatimaye kupata mavuno mengi ya kujivunia ukilinganisha na kilimo cha awali.

# JINSI YA KUANDAA MBEGU ZA MPUNGA

*Kitengo cha Kilimo bora cha mpunga-KATC*

Wakulima wengi wa mpunga wamekuwa wakitumia mbegu nyingi za mpunga ambazo huoteshwa na kupandwa bila kufahamu mahitaji halisi na kusababisha uharibifu wa mbegu usio wa lazima. Aidha miche ambayo hutokana na mbegu hizo huwa midhaifu na hivyo huchangia kuathiri uzalishaji. Hayo yote husababishwa na wakulima kutokujua mbinu bora za kitaalamu za utayarishaji wa mbegu za mpunga.

Ili kupata mbegu nzito na zilizojaa vizuri, hatua zifuatazo zinashauriwa zifuatwe: Kabla ya kusia mbegu kwenye kitalu, pembua na loweka.mbegu ili kuondoa mapepe na kupata mbegu zilizojaa vizuri. Kuna njia mbili za kupembua mbegu nazo ni : kupembua kwa kutumia maji safi na kupembua kwa kutumia maji safi na chumvi. Katika njia hizo mbili; njia ya kupembua kwa maji yenye chumvi, ndiyo inayopendekezwa na wataalamu. Njia hii husababisha kiasi kikubwa cha mapepe kutoka ambayo yasingeweza kuondolewa kwa kupepeta au kwa kutumia maji safi peke yake.

### Jinsi ya kupembua mbegu kwa kutumia maji safi pamoja na chumvi

**Mahitaji:** - Chumvi kilo 2, Maji lita 10, Yai la kuku, Kijiti cha kukorogea - Chombo cha kupembulia na kuwekea mbegu (ndoo,beseni).

### Jinsi ya kupembua:

-Changanya maji na chumvi kisha koroga vizuri

-Weka yai kwenye maji ya chumvi

Kama yai litaelea juu ya maji ina maana kuwa mchanganyiko unafaa. Kama halikuelea ongeza kiasi cha chumvi.

-Toa yai na weka mbegu kwenye maji yenye chumvi

-Koroga kwa kijiti na acha maji yatulie na mapepe yaelee juu

-Ondoa mapepe na endelea kukoroga na kuondoa mapepe mpaka yaishe

-Osha mbegu kwa maji safi mara tano ili kuondoa chumvi

-Loweka mbegu kwa kutumia maji safi

**Madhumuni ya kuloweka mbegu ni kuiwezesha mbegu kunyonya maji ya kutosha ili iweze kuchipua kabla ya kusia kwenye kitalu.**

### Jinsi ya kuloweka mbegu:

Kuna njia mbili za kuloweka mbegu (1) Kuloweka mbegu kwenye maji kwa siku nne (4) mfululizo huku ukibadilisha maji, (2) Kuloweka mbegu kwenye maji kwa masaa 24 yaani siku moja na baadaye kutolewa na kuatamishwa kwa masaa 48. Katika njia hizi mbili, njia ya kuloweka mbegu mfululizo kwa siku nne ndiyo inayopendekezwa. Njia hii imeonekana ni bora zaidi kutokana na sababu zifuatazo:-

- Mbegu zote huota kwa pamoja
- Hata kama siku zitazidi kabla ya kusia kwenye kitalu hakutakuwa na madhara kwani ukuaji wa mbegu ni wa polepole.
- Hakuna uwezekano wa mche midogo kuvunjika wakati wa kusia kwenye kitalu hasa wakati wa kufunika mbegu kwa kupigapiga na viganja.
- Usiaji wa mbegu kwenye kitalu huwa ni rahisi kwani mbegu huwa hazina mizizi iliyoshikamana.

### Jambo la kuzingatia:

Maji yabadilishwe kila baada ya masaa 12 ili mbegu zisioze kwa kukosa hewa safi.

### Kiasi cha mbegu kwa eneo

Kilo 20-22 za mbegu iliyotayarishwa vizuri hutosha kwenye shamba lenye ukubwa wa hekari moja. Kiasi hicho kinaweza kusiwa kwenye kitalu chenye matuta 10 yenye urefu wa mita 15na upana wa mita 1.5 kila tuta. Hivyo basi kilo 2 za mbegu zinatosha kusiwa kwenye kitalu/tuta lenye ukubwa uliotajwa hapo juu.

Kiasi hicho kimekadiriwa kwa upandikizaji wa nafasi ya sm. 30 kwa sm.15 na kupanda miche 3 kwa shina.

Kama mbegu haikuandaliwa vizuri, kiasi cha mbegu kinaweza kufikia kilo 30– 40 kwa hekari.



Baada ya kuziweka mbegu zako kwenye maji yaliyotiwa chumvi, endelea kukoroga ili mapepe yote yaelee



Ondoa mapepe yote yanayoelea



Mbegu zilizoatamishwa kwa masaa 48



Mbegu ambazo hazikuatamishwa bali zililowekwa kwa siku 4 mfululizo